

NIPAJHE JUMAMUOSI, FEBRUARI 10, 2024 UK. 15

Taasisi zaagizwa kuendeleza 4R

Na Cynthia Mwilolezi,
ARUSHA

TAASISI za Serikali zimeagizwa kuendeleza falsafa ya Rais Samia Hassan Suluhu ya 4R kutoa huduma kwa wananchi haraka kupitia Serikali Mtandao (e-GA).

Agizo hilo lilitolewa jana jijini hapa na Naibu Waziri Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Ridhiwani Kikwete wakati akifunga kikao kazi channe cha e-GA.

Rudhiwani aliwasisitiza maofisa wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) kufanya matumizi sahihi ya mtandao ili kuharakisha maendeleo kwa serikali na taasisi zake.

Alisema ni lazima e-GA izingatie sheria, viwango na

sera kwa ajili ya ubadilishanaji taarifa za serikali salama. "4R ya Rais wetu ya kuhimiza ustahamilivu siyo kwa wanasiasa pekee bali kila nyanja kwa sababu mageuzi na ujenzi mpya wa maridhiano ni nguzo muhimu katika uletaji chachu ya maendeleo nchini, kuondoa changamoto za wananchi kupitia mifumo inayosomana na naziagiza taasisi za umma kusomana kupitia mifumo ya kidigitali," alisema.

Alisema kuna watu wanatumia barua pepe zisizo rasmi kutapeli wananchi katika ajira na malipo, hivyo wataalamu wa TEHAMA hasa serikali mtandao wanatakiwa kuwa kwa makini ili kuhakikikisha usalama wa mtandao unadhibitiwa.

"Kama kuna changamoto ya mifumo kutosomana ni wa-

jibu zizungumzwe kuondoa ukakasi huo na kwenda pamoja katika ujenzi wa kidigitali, ikiwamo maofisa masuhuli kuwajengea uwezo wataalamu wa serikali kufikia malengo ya kidigitali," alisema.

Alisema serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ya kuhakikisha e-GA inafikia malengo na kutoa ufanisi wa kidigitali kupitia mfumo huo.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya e-GA, Benedict Ndomba, alisema miradi ikiwa na mifumo ya TEHAMA, itasaidia kuokoa fedha za umma na za serikali.

"Tunamshukuru Rais Samia Hassan Suluhu kwa kujenga serikali kidigitali, lakini naomba Serikali kuweka mazingira wezeshi kwa e-GA katika kuleta ufanisi zaidi,"

alisema.

Mkurugenzi wa e-GA Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), Said Seif Said, alipongeza ushirikiano baina Zanzibar na Tanzania Bara kwa ajili ya kuhakikisha utendaji kazi ofisini unakuwa kwa kasi kupitia teknolojia hizo. Akisoma maazimio yaliyofikiwa kwenye kikao kazi hicho, Priscas Kiwango kuwa ni pamoja na kila taasisi kuteua ofisa TEHAMA kusimamia miongozo na kanuni za usimamizi bora wa mtandao, taasisi za umma ziboreshe na kutumia teknolojia hiyo.

Nyingine ni utoaji huduma kwa wananchi, kufanya tathmini ya hali ya TEHAMA, uundaji wa ripoti katika kila taasisi husika na kuwasilisha e-GA kabla ya mwaka wa fedha.